# MAPENDEKEZO YA NAMNA BORA YA UTEKELEZAJI WA TAARIFA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA MALALAMIKO KATI YA WANANCHI NA MGODI WA DHAHABU WA NORTH MARA

**MAPENDEKEZO YA NAMNA BORA YA UTEKELEZAJI WA TAARIFA YA KAMATI YA KUCHUNGUZA MALALAMIKO KATI YA WANANCHI NA MGODI WA DHAHABU WA NORTH MARA**

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| **A: Fidia Mbalimbali za Ardhi** | | | | |
| 1 | Malalamiko ya watu 15 wanaodai kwamba walilipwa fidia pungufu | Fidia hizo zilifanyika kulingana na uthamini na wafidiwa walikubaliana na kupokea fidia stahiki kwa wakati huo. Kamati imebaini kuwa malipo hayo yalifanyika kisheria, hivyo suala hili halistahili mjadala zaidi na hivyo limefungwa. | Suala hili limefungwa | • Wananchi wanaodai mapunjo ya fidia<br>• Mgodi<br>• Kamati ya Utekelezaji |
| 2 | Maeneo ambayo Mgodi ulitangaza kuchukua maeneo na baadae kuachana na mpango huo (Eneo la Mrwambe) | Mgodi hauwezi kulazimishwa kuchukua maeneo ambayo hauyahitaji, hivyo maeneo hayo yanabaki chini ya umiliki wa wananchi. Kwa kuwa eneo hilo lilifanyiwa tathimini na wananchi hao kuzuiliwa kuendeleza | 19/07/2016 hadi 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Halmashauri ya Wilaya<br>• Wananchi<br>• Kamati ya utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | makazi yao, Kamati inapendekeza kuwa wananchi ambao walikuwa hawajalipwa fidia, walipwe fedha ya usumbufu kwa mujibu wa sheria kwa kuzingatia uthamini uliofanyika kwa wakati husika.<br>Kwa mujibu wa sheria, fidia ya usumbufu ni asilimia 8 ya fidia kuu. Kamati inapendekeza Mgodi ulipe asilimia 16 ya fidia kuu ambapo asilimia 8 ilipwe kwa mwananchi anayepaswa kufidiwa na asilimia 8 inayosalia ilipwe Serikali ya Kijiji kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Kijiji. | | |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Malalamiko ya wananchi wa Kijiji cha Nyakunguru (kitongoji cha Nyamichele) – ambao maeneo yao yalifanyiwa uthamini, mazao yao kufyekwa na walizuiwa kuendeleza maeneo yao. | • Mgodi hauwezi kulazimishwa kuchukua maeneo ambayo hauna uhitaji nayo. Kwa kuwa kuna mazao yalifyekwa na wananchi walizuiwa kwa muda kuendeleza maeneo yao na hivyo kupata usumbufu, kwa mazao yaliyofyekwa, Kamati inapendekeza Mgodi ulipe fidia kwa viwango vya upandaji bora wa mazao *(Agricultural best practice)* na fidia ya usumbufu.<br><br>• Kwa mujibu wa sheria, fidia ya usumbufu ni asilimia 8 ya fidia kuu ya mali inayohusika (Fidia ya Mazao). Kwa kuwa wananchi walizuiliwa | 19/07/2016 hadi 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Wizara ya Nishati na Madini<br>• Wizara ya Ardhi<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | kulima mashamba yao kwa muda mrefu, Kamati inapendekeza kiwango cha fidia kiongozwe kwa kuutaka Mgodi ulipe asilimia 50 ya fidia kuu. Kamati inapendekeza kuwa katika asilimia hizo 50, asilimia 25 ilipwe kwa mwananchi anayepaswa kufidiwa na asilimia 25 inayosalia ilipwe kwenye Serikali ya Kijiji kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Kijiji.<br><br>• Kwa wananchi 19 waliofanyiwa uthamini wa nyumba walipwe fedha ya usumbufu wa asilimia 8 ya thamani ya uthamini wa nyumba. | | |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Wananchi waliofanyiwa uthamini mwaka 2011/2012 katika vijiji vya Mjini Kati na Nyabichune na wakakataa kuchukua malipo yao. | • Kamati inapendekeza wananchi wanaohusika wachukue malipo yao katika kipindi cha wiki tatu kuanzia tarehe 19/07/2016. Kwa watakaokuwa hawajachukua malipo yao katika muda huo, hundi za malipo yao zipelekwe Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa matunzo hadi hapo zitapokuja kuchukuliwa na wahusika. Baada ya hapo Serikali ichukue hatua ya vunja nyumba na kusafisha eneo linalohusika ili kuruhusu shughuli za Mgodi kuendelea.<br><br>• Wananchi ambao watakuwa na malalamiko ya uthamini na fidia wawasilishe malalamiko yao Mgodini na | 19/07/2016 hadi 07/08/2016 | • Wizara ya Nishati na Madini<br>• Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maenedeleo ya Makazi<br>• Mgodi<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | wakishindwa kuelewana wapeleke malalamiko yao kwa Kamishina wa Madini | | |
| 5 | Wananchi ambao walikataa kufanyiwa uthamini mwaka 2011/2012 katika vijiji vya Mjini kati na Nyabichune. | Kamati inapendekeza Mgodi ufanye uthamini wa mali zao ndani ya wiki tatu kwa kuzingatia hali ya mali hizo kwa Mwaka 2012. Endapo wataendelea kukataa mali zao kufanyiwa uthamini, Serikali ifanye uthamini kwa mujibu wa sheria kwa kuzingatia hali ya mwaka 2012 na kulipa fidia kwa viwango vya Serikali. | 19/07/2016 hadi 07/08/2016 | • Wizara ya Nishati na Madini<br>• Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi<br>• Mgodi<br>• Kamati ya Utekelezaji |
| 6 | Wananchi walio ndani ya eneo la Hekta 47 za Kijiji cha Matongo ambao walipaswa kufanyiwa uthamini mwaka 2014 | Kamati inapendekeza uthamini ufanyike kwa mujibu wa hali halisi ya mwaka 2014.<br>Aidha, Kamati ilibaini kuwa Mgodi ulitoa ahadi ya kulipa Shilingi Millioni 500 kwa Serikali ya Kijiji. Kamati inapendekeza ahadi hiyo itekelezwe sambamba na malipo ya fidia. | 19/07/2016 hadi 07/08/2016 | • Wizara ya Nishati na Madini<br>• Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi<br>• Mgodi<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| 7 | Watu walio ndani ya mita 200 ya eneo hai la shughuli za Mgodi | Kamati inapendekeza Wananchi walioko ndani ya mita 200 ya eneo hai la shughuli za Mgodi wahamishwe kwa mujibu wa sheria kwa kuzingatia picha za Satellite za mwaka 2014. | Zoezi likamilike ifikapo tarehe 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Halmashauri ya Wilaya<br>• Wananchi<br>• Kamati ya Utekelezaji |
| 8 | Wananchi waliotegesha (Kujenga nyumba kwa utitili katika eneo moja madai ya kuongeza thamani kwa lengo la kujipatia fidia kinyume cha sheria, kanuni na taratibu) | Kamati inapendekeza wananchi hao wasilipwe chochote kwa kuwa kitendo hicho ni kinyume na sheria. Mamlaka husika ziendelee kusimamia sheria ili vitendo hivyo visijitokeze tena. | | • Mgodi<br>• Halmashauri ya Wilaya ya Tarime<br>• Wananchi<br>• Serikali za Vijiji<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| **Fidia zinazohusu madhara kwa Binadamu na Mifugo** | | | | |
| 9 | Wananchi wenye malalamiko juu ya madhara waliyopata kutokana na shughuli mbalimbali za Mgodi kama vile milipuko, athari za vumbi, maji, na mifugo kufa kwa madai ya kutumia maji yaliyochafuliwa na shughuli za Mgodi. | Kamati inapendekeza malalamiko yenye ushahidi yapelekwe Mgodini ili yafanyiwe kazi ikiwa ni pamoja na kulipwa fidia zao pale inapostahili na kukubalika. Ikishindikana yapelekwe kwa Kamishina wa Madini kwa mujibu ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. | Ifikapo tarehe 30/09/2016 | • Wizara ya Nishati na Madini<br>• Mgodi<br>• Kamati ya Utekelezaji |
| 10 | Malalamiko ya wananchi wa Kijiji cha Komarera dhidi ya Mgodi. | Kamati inapendekeza wananchi wenye malalamiko wayawasilishe kwenye uongozi wa Mgodi ili yashughulikiwe. Wasipoafikiana, wahusika wapeleke masuala yao kwa Kamishina wa Madini. | Ifikapo 07/08/2016 | • Mgodi<br>• Kamishina wa Madini<br>• Wananchi<br>• Kamati ya utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| **B. Kuhusu tuhuma mbalimbali zinazohusu Jeshi la Polisi kuonea watu na kuuwa watu** | | | | |
| 11 | Malalamiko 335 ya watu wanaodai kuonewa na kuteswa na Jeshi la Polisi, malalamiko 65 ya watu wanaodai kuuwawa na Polisi na malalamiko 270 ya watu wanaodai kujeruhiwa na Polisi. | Kamati ilipokea malalamiko husika. Hata hivyo haikuwa na mamlaka ya kimahakama ya kuweza kuthibitisha usahihi wa madai hayo bila shaka yoyote. Hivyo, Kamati inapendekeza yafuatayo:-<br><br>• Mamlaka za nidhamu za Jeshi la Polisi zisimamie utendaji na nidhamu ya Askari wanaofanya kazi maeneo ya Mgodi na kuweka utaratibu wa kupokea na kufanyia kazi malalamiko ya kimaadili dhidi ya Askari hao na kuchukua hatua stahiki.<br><br>• Kamati imebaini | Ifikapo tarehe 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Kamati ya Ulinzi na Usalama<br>• Serikali ya Vijiji<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | kumekuwepo na matukio mengi ya uvamizi wa Mgodi na uvunjaji wa sheria. Kamati inashauri, ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kutokana na vitendo hivyo wananchi wanaaswa kuzingatia sheria bila shuruti na kudumisha mahusiano mazuri kati yao na Jeshi la Polisi na Mgodi.<br><br>• Kwa wahusika wenye ushahidi wapeleke malalamiko yao Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kesi zifunguliwe dhidi ya Polisi waliohusika.<br><br>• Ili kupunguza uhalifu kwenye maeneo | | |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | yanayozunguka Mgodi, Jeshi la Polisi liimarishe programu ya ulinzi shirikishi kwa kuanzisha vikundi vya ulinzi. Aidha katika utekelezaji huo, Mgodi na vijiji vishirikiane kusimamia. | | |
| **C. Uchafuzi wa vyanzo vya maji na uharibifu wa Mazingira** | | | | |
| 12 | Wachenjuaji wadogo wa dhahabu katika kijiji cha Kerende kuchafua vyanzo vya maji | Baada ya Kamati kutembelea maeneo hayo ilibaini kuwa uchenjuaji ulikuwa unafanyika katika mabonde ambayo kipindi cha mvua hutiririsha maji kwenda sehemu mbalimbali za vyanzo vya maji. Kamati inapendekeza kuwa shughuli za uchenjuaji madini zifanyike kwa kuzingatia taratibu za uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira. Hivyo shughuli za uchenjuaji wa | Ifikapo 30/08/2016 | • Wizara ya Maji na Umwagiliaji<br>• Halmashauri<br>• Kampuni za uchenjuaji<br>• Wachenjuaji binafsi<br>• Serikali za Vijiji/Vitongoji<br>• Kamati ya Utekelezaji. |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | madini kwenye vyanzo vya maji zisitishwe na wachenjuaji waamuliwe kuondoka kwenye vyanzo vya maji. | | |
| 13 | Uchimbaji wa dhahabu chini ya ardhi (underground mining) kuathiri visima vya maji katika Kijiji cha Komarera | Kamati inapendekeza kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Nishati na Madini kutuma wataalam kubaini chanzo halisi cha kukauka visima katika Kijiji hicho na kupendekeza hatua stahiki za kuchukuliwa kwa kile kitakachobainika. | Ifikapo 30/08/2016 | • Wizara ya maji na umwagiliaji<br>• Wizara ya Nishati na Madini<br>• Mgodi<br>• Halmashauri<br>• Wananchi |
| 14 | Mafuriko ya Mto Tighite kuathiri mashamba ya wananchi kutokana na kuhamishwa kwa njia yake ya asili ili kupisha uchimbaji katika shimo la dhahabu la Nyabigena | Kamati haikuweza kuthibitisha kama mafuriko hayo yalisababishwa na kuhamishwa kwa Mto Tighite. Hivyo, Kamati inapendekeza mamlaka husika kuchunguza suala hili. | Ifikapo 30/12/2016 | • Wizara ya Maji na Umwagiliaji<br>• Wizara ya Nishati na Madini<br>• Mgodi<br>• Halmashauri<br>• Serikali za Vitongoji /Kijiji<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 15 | Malalamiko ya wananchi kuwa wanaathirika kiafya na maji ya Mto Tighite, TSF na vyanzo vya maji vya asili.<br>• Kamati ilichukua sampuli za maji 113 kwa ajili ya uchunguzi wa maabara kwa Vipimo vya mahalia (physical parameters), metali (chemical parameters) na vimelea vya vijidudu (microbiology).<br>• Matokeo ya uchunguzi wa Mkemia Mkuu wa Serikali yalibaini kuwa:-<br>*Kutoka Mto Tigithe*<br>- Cadmium | Vipimo vya manganese na chuma katika Mto Tighite vilibainika kuwa juu ya viwango. Hali hii inaweza kuwa imechangiwa na jiolojia ya eneo husika. | | • Halmashauri ya wilaya<br>• Wizara ya Maji<br>• Wizara ya Afya<br>• Mgodi<br>• Serikali za Vijiji<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | - Arsenic<br>- Lead<br>- Cyanide<br>Parameters tajwa hapo juu vilikuwa ndani ya viwango vinavyokubalika kitaifa.<br><br>- Manganese (Vipimo vilionyesha 0.53mg/l ambapo kiwango cha TBS ni 0.5mg/l hivyo Mn ilizidi kwa kiwango chaa 0.03mg/l)<br><br>- *Iron* (vipimo vilionyesha kuwa kati ya 2.033 – 4.475mg/l ambavyo ni juu ya Viwango vya TBS (1.0mg/l)<br><br>Sampuli kutoka | | | |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | *TSF* na maeneo yanayozunguka *TSF*<br>- *Arsenic* (ilionekana kuwa kati ya 0.257 – 0.284mg/l ambapo ni juu ya kiwango cha TBS cha 0.20mg/l)<br><br>- *Iron* (chuma)- Sampuli toka *North TSF Sump* Barabarani (1.888mg/l) na TSFBH04S (3.424mg/l) vilikuwa juu ya viwango vya TBS (1.0mg/l)<br><br>Vipimo vya vimelea vya vijidudu *(microbiology)* | • Kuonekana kwa vijidudu kwenye maji ni kiashiria kuwa uchafuzi wa maji umetokana na ama | | |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | - Sampuli za mto Tigithe na visima vya maji vilionyesha uwepo wa vimelea vya vijidudu (bacteria)- (E.coli na Total coliforms) | vinyesi vya binadamu au mifugo. Hivyo uchafuzi huo unaweza kupelekea magonjwa ya kuhara na maumivu ya tumbo. Kutokana na hali hiyo Kamati inapendekeza wananchi kutibu maji ya kunywa kabla ya kuyatumia. Pia ufuatiliaji wa ubora wa maji utiliwe mkazo.<br><br>• Kamati inapendekeza Wizara ya Afya itume wataalam kuchunguza malalamiko ya wananchi wanaodai kuathirika kiafya kutokana na shughuli za Mgodi. | | |
| 16 | Mashamba na mifugo kuathiriwa na maji ya Mto Tighite pamoja na mifugo kuugua ugonjwa wa ngozi | Kamati ilibaini baadhi ya mifugo kuugua magonjwa ya ngozi. Hata hivyo, Kamati haikuweza kuhusisha maradhi hayo na hali ya maji ya Mto Tighite kwa | Ifikapo tarehe 30/09/2016 | • Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi<br>• Halmashauri<br>• Wananchi<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | kuwa suala hili lilihitaji uchunguzi wa kitaalam zaidi. Kwa misingi hiyo, Kamati inapendekeza watalaam wa Kilimo na Mifugo kutumwa ili kubaini tatizo halisi. | | |
| 17 | Ubora wa maji ya mvua katika vijiji vya Matongo na Mjini Kati kuathiriwa na teknolojia ya kupampu maji hewani *(Forced Evaporation)* kutoka TSF. | Kazi ya Kamati kwa suala hili ilifanyika katika kipindi cha kiangazi na hivyo kutokupata maji ya mvua ili kuyachunguza. Kamati inapendekeza kuwa wataalam wa ubora wa maji kwa kushirikia na Halmashauri pamoja na Mgodi wafanye ufuatiliaji kipindi cha mvua ili kubaini hali halisi ya tatizo. | Msimu ujao wa mvua | • Wizara ya Maji na Umwagiliaji<br>• Halmashauri<br>• Mgodi<br>• Serikali za Vijiji<br>• Kamati ya Utekelezaji |
| | **D. Utengaji wa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo** | | | |
| 18 | Kupatikana kwa maeneo ya wachimbaji wadogo. | Wizara ya Nishati na Madini imebainisha eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 7.69 (sawa na hekta 769) katika | Ifikapo 15/10/2016 | • Uongozi wa Mkoa / Wilaya<br>• Wizara ya Nishati na Madini |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | kijiji cha Kewanja. Eneo hili lote likigawiwa leseni ndogo cha uchimbaji wa madini PML zenye ukubwa wa hekta 10 kila moja, linaweza kutoa leseni 76. Hata hivyo, eneo hilo litafanyiwa kwanza uchunguzi wa kijiologia na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) kabla kugawa leseni. Kazi ya uchunguzi wa kijiolojia na kutoa leseni kwenye maeneo yatakayoonekana yanafaa.<br><br>Aidha, katika kijiji cha Kerende limetengwa eneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo lenye ukubwa wa hekta 598 ambapo leseni 96 zimeshatolewa na bado kuna hekta 79 zimebaki hadi sasa kwenye eneo hilo. Maeneo mengine yaliyotengwa | | • Wizara ya Ardhi<br>• Serikali za Mitaa<br>• MEM<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | jirani na Mkoa wa Mara ni pamoja na Ilujamate-Misungwi, Mwanza (hekta 147), Nyangarata-Kahama, Shinyanga (Hekta 1074), Ibologelo-Igunga, Tabora (Hekta 6,527) ambayo yametengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Yeyote mwenye uhitaji afike ofisi za madini zinazosimamia maeneo hayo. | | |
| | **E. Upatikanaji wa mawe wa dhahabu (Magwangala)** | | | |
| 19* | Kupatikana Mawe (Magwangala) kwa ajili ya wananchi wa maeneo yanayozunguka Mgodi | Katika kutekeleza suala hili mambo yafuatayo yanatakiwa yatekelezwe :<br>- Serikali ya Wilaya na vijiji ibainishe maeneo kwa ajili ya wananchi | Ifikapo tarehe 30/10/2016 | • Viongozi wa Vitongoji / Vijiji vinavyohusika<br>• Mkuu wa Wilaya<br>• Mgodi<br>• NEMC |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | | kumwagiwa magwangala ;<br><br>- Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) itafanyia Thathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa eneo lililotengwa. Kazi hizo za utengangaji wa maeneo ya kumwaga magwangala pamoja na tathmini ya athari za mazingira zinatakamika.<br><br>- Majadiliano yatafanyika kati ya Mgodi, Wilaya na Serikali za vijiji kuhusu namna bora ya kusafirisha magwangala kutoka Mgodini hadi eneo lilotengwa ;<br><br>- Serikali ya Wilaya na Vijiji vitawajibika | | |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | | kusimamia usalama na ongezeko la watu wakati wa uchukuaji wa magwangala kutoka eneo lililotengwa ;<br>- Hata hivyo, itabidi kufanya uchunguzi wa kiwango cha dhahabu katika magwangala ilikuona kama magwangala hayo yatakuwa na manufaa kwa wananchi. | | |
| **F. Fursa za Biashara na Ajira kwa wazawa wa Tarime na wananchi wanaozunguka Mgodi** | | | | |
| 20 | Fursa za Biashara :<br><br>Kamati ilibaini kwamba kuna Makampuni 21 yanayomilikiwa na Watanzania yanayofanya biashara na Mgodi. | Mgodi uendelee kutoa fursa za biashara kwa Makampuni ya Wazawa ili kuyajengea uwezo zaidi. | Endelevu | • Mgodi<br>• Halmashauri<br>• Wananchi |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | Kati ya hayo, Makampuni 11 yanamilikiwa na wenyeji wa Nyamongo. | | | |
| 21 | Fursa za ajira na watanzania kujiendeleza<br><br>Kamati ilibani kuwa kuna jumla ya waajiriwa 2,214 wa Mgodi na Wakandarasi ambapo watanzania ni 2094 (sawa na asilimia 94.6). Aidha katika Kampuni ya North Mara pekee kuna wafanyakazi wazawa 968 na kati ya hao, waajiriwa 237 ambao ni sawa | Mgodi na Wakandarasi waendelee kutoa kipaumbele za fursa za ajira kwa watanzania | | • Mgodi<br>• Wakandarasi<br>• Halmashauri ya Wilaya<br>• Wananchi |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | na asilimia 26 wanatokea Nyamongo. | | | |
| | **G. Kuhusu Kesi zilizopo Mahakamani na Uwezekano wa Usuluhishi** | | | |
| 22 | Kamati ilibaini kuwa kuna kesi **15** kati ya Mgodi na wananchi ambazo ziko mahakamani na hazijatolewa maamuzi. Hali hii inaleta misuguano kati ya Mgodi na Wananchi na hivyo kuleta mahusiano mabaya. | Kamati inapendekeza kesi hizo zisimamishwe mahakamani ili ufanyike usuluhishi nje ya Mahakama. Usuluhishi ukishindikana, kesi ziendelee kusikilizwa Mahakamani. | Ifikapo tarehe 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Wananchi<br>• Kamati ya utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | **H. Mikataba (VBA) na utoaji wa huduma za kijamii (CSR)** | | | |
| 23 | Utekelezaji wa VBA :<br>Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa mikataba ulikuwa hauendi kulingana makubaliano ya mikataba husika | Kamati inapendekeza Mgodi uongeze kasi ya utekelezaji wa mikataba kulingana na matakwa ya mikataba. Aidha, Halmashauri isimamie kwa karibu utekelezaji wa mikataba hiyo | Miradi ikamilike mpaka 30/12/2017 | • Mgodi<br>• Halmashauri<br>• Wananchi<br>• Kamati ya utekelezaji |
| 24 | Huduma za kijamii (Corporate Social Responsibility-CSR) :<br>Kamati ilibaini kuwepo kwa mawasiliano yasioridhisha kati ya wananchi na Mgodi kwenye miradi inayotekelezwa | Halmashauri ishiriki ipasavyo katika uibuaji, upangaji wa utekelezaji na usimamizi wa miradi inayotegezwa kupitia CSR | Endelevu | • Halmashauri ya Wilaya ya Tarime<br>• Mgodi<br>• Wananchi<br>• Kamati ya utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | kupitia CSR | | | |
| 25 | Mwelekeo wa Mgodi wa chini ya ardhi na athari zake kwa vijiji na leseni zenye mikataba na Mgodi :<br><br>Kamati ilibaini kuwa maeneo ya leseni saba zenye mikataba ya uchimbaji na Mgodi yako umbali wa takribani mita 300 kutoka mahali uchimbaji wa chini ya ardhi unapoendeshwa. Hata hivyo mashapo ya Mgodi unaochimbwa chini ya ardhi hayaelekei upande wa maeneo | Kamati inapendekeza Wizara ya Nishati na Madini iwe inafanya ufuatiliaji wa uchimbaji wa chini ya ardhi ili kubaini uchimbaji huo umefika wapi ili kuthibiti mwenendo wa uchimbaji huo. | Endelevu | • Wizara ya Nishati na Madini<br>• Mgodi<br>• Serikali za vijiji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | ya leseni hizo. | | | |
| **I.** | **Mengineyo** | | | |
| 26 | Nyumba zinazolalamikiwa kujengwa na Mgodi chini ya kiwango. | Kamati ilibaini kuwa baadhi ya nyumba zilionekana kuwa na nyufa na sakafu kubomoka.<br><br>Kamati inapendekeza wananchi waliojengewa nyumba hizo kuwasilisha malalamiko yao Mgodini ili Mgodi uzikarabati. | Ifikapo tarehe 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Wananchi<br>• Kamati ya Utekelezaji<br>• Halmashauri ya Wilaya ya Tarime |
| 27 | Matengenezo ya barabara inayopita katika vijiji vya Nyakunguru – Nyarwana – Weigita-Nkerege – Komaswa inatumiwa na Mgodi kupitishia magari ya | Kamati inapendekeza Halmashauri na Mgodi wakae pamoja na kuweka mkakati wa kuitengeneza. | Wawe wamekaa ifikapo tarehe 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Halmashauri ya Wilaya ya Tarime<br>• Mbunge<br>• Kamati ya Utekelezaji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | mizigo. | | | |
| 28 | Upatikanaji wa maji safi na salama ya matumizi ya wakaazi wa Kata ya Matongo na Kemambo | Kamati inapendekeza :<br>• Mgodi uendeleze chanzo cha uhakika kilichofanyiwa utafiti na Mgodi katika eneo la Mlima Sukube (Kijiji cha Kewanja)<br>• Serikali za vijiji zihusike kwenye ulinzi wa miundombinu ya maji ili isiharibiwe. | Ifikapo Desemba 30 2017 | • Halmashauri ya Wilaya ya Tarime<br>• Mgodi<br>• Serikali ya Kijiji cha Matongo na Kemambo<br>• Kamati ya Utekelezaji |
| 29 | Uendelevu wa miradi ya maji inayowekezwa vijiji vinavyozunguka Mgodi. | Taarifa kutoka Mgodini ilionesha kuwa vijiji vinavyozunguka Mgodi vina visima vipatavyo 52. Hata hivyo, taarifa ya Halmashauri ya Wilaya ilibainisha kuwa kuna | 30/09/2016 | • Halmashauri ya Wilaya ya Tarime<br>• Wizara ya Maji na Umwagiliaji<br>• Serikali ya kijiji |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | changamoto katika usimamizi na uendelevu wa vyanzo vya maji.<br><br>Kamati inapendekeza kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Halmashauri zikae na kubaini namna bora ya uendelevu wa miradi katika vijiji hivyo. | | • Mgodi<br>• Wananchi |
| 30 | Mgogoro wa mkataba wa fidia kati ya Mgodi na Kijiji cha Nyangoto (suala la asilimia 5) | Kamati inapendekeza Mkurugenzi wa Halmashauri akutanishe pande mbili zinazohusika ili kufikia muafaka juu ya suala hili. | Ifikapo 30/09/2016 | • Mgodi<br>• Mkuu wa Wilaya ya Tarime<br>• Serikali ya Kijiji cha Nyangoto<br>• Kamati ya utekelezaji |
| 31 | Wachimbaji wadogo waliokuwa wanachimba kwenye leseni za uchimbaji mdogo wa vijiji | Kamati inapendekeza kuwa wachimbaji hao waende kwenye serikali za vijiji walipokuwa wanachimba ili waweze | | • Serikali za vijiji<br>• Wachimbaji wanaodai |

| NA | HOJA | MAPENDEKEZO | MUDA WA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | vitano (5) eneo la Nyabigena | kupata muafaka wa jambo hili. | | |
| 32 | Wachimbaji wadogo wa dhahabu eneo la Nyabirama walioingia mkataba wa uchimbaji wa asilimia moja na Kampuni ya Afrika Mashariki Gold Mine ambayo maeneo yao hayafanyiwi uchimbaji na maeneo hayo kuwekewa miundombinu ya Mgodi | Kamati inapendekeza kuwa wachimbaji hao wawasilishe malalamiko yao Mgodini ili yashughulikiwe na kupata ufumbuzi. Endapo hawataelewana, wawasilishe malalamiko yao kwa Kamishna wa Madini | 30/09/2016 | • Wanachimbaji wadogo<br>• Mgodi<br>• Wizara ya Nishati na Madini<br>• Kamati ya utekelezaji |